HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KWENYE UFUNGUZI WA MKUTANO WA MWAKA WA WATAYARISHAJI VIPINDI VYA ELIMU KWA UMMA

TAREHE 20 FEBRUARI, 2024

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji Tanzania,
Mwenyekiti wa Bodi ya TBC,
Wajumbe wa menejimenti ya TBC,
Wajumbe wa Mkutano,
Waandishi wa Habari,

Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!!!!!

Wageni waalikwa, mabibi na mabwana.

Awali ya yote napenda kuwapongeza wajumbe wote kwa ushiriki wenu katika Mkutano wa mwaka wa Watayarishaji wa Vipindi vya Elimu kwa Umma. Huu ni mkutano muhimu na wa kipekee kabisa ambao unatoa fursa kwa watayarishaji wa vipindi vya elimu kwa umma kwa njia ya redio na televisheni kupata mafunzo na kubadilishana uzoefu.

Ndugu Wajumbe na wageni waalikwa,

Napenda pia kumpongeza Mkurugenzi Mkuu wa TBC, Dkt. Ayub Rioba Chacha, Menejimenti na jumuiya yote ya TBC kwa kuandaa mkutano hu.

Aidha, niwashukuru wadhamini wote kwa kukubali kudhamini mkutano huu muhimu. Wadhamini hao ni **TPA, STAMICO, GOLD CREST HOTEL, EWURA, RUWASA, OSHA, TPDC, SUZA, TCRA, CHAMA CHA WAUGUZI TANZANIA, eGA- ZANZIBAR, MoCU, e-GA, NSSF, UCSAF, AICC, NIC, WCF, CHUO CHA MIPANGO, ATCL, ROYAL DIAMOND HOTEL NA CHUO CHA WANYAMA PORI** PASIANSI. Kwa kudhamini mkutano huu mmechangia kwa namna ya kipekee katika kuwaongezea ujuzi watoa elimu kwa Watanzania kwa njia ya redio, televisheni na mitandao ya kijamii.

Ndugu Wajumbe na wageni waalikwa,

Mkutano huu unawapa washiriki fursa ya kutafakari masuala mbalimbali kuhusu maendeleo ya wananchi . Aidha, ni matumaini yangu kuwa kupitia Mkutano huu wenye kauli mbiu ya **"Vyombo vya Habari na Falsafa ya R4"** mtajifunza mambo mengi kutokana na mada mbalimbali zitakazowasilishwa ili muweze kuwahabarisha wananchi kuhusu mambo mbalimbali ikiwemo miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali.

Ndugu Wajumbe na wageni waalikwa,

Dira na malengo ya Sera ya Habari na Utangazaji ni kuwepo kwa vyombo vingi vya habari, imara na anuwai na vyenye kuzingatia maadili ya taaluma na ya jamii ili viweze kuchangia katika kufanikisha malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na Dira mpya ya Maendeleo ya Taifa 2050. Kwa mantiki hiyo, kuwepo kwa vyombo vya habari vilivyo imara na vinavyozingatia maadili ya taaluma, kutachangia kuondoa vikwazo vinavyokwamisha upatikanaji wa haki

ya wananchi ya kupokea na kupata habari na hivyo kuchangia katika kufanikisha malengo ya Taifa na kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu shughuli zinazofanywa na Serikali yao.

Ndugu Wajumbe na wageni waalikwa,

Sote tunafahamu kuwa wanahabari mna jukumu kubwa katika kuhamasisha na kuwashawishi wananchi katika juhudi zao za kuleta mabadiliko ya kimaendeleo katika maisha yao ya kila siku na kubeba falsafa na maono ya viongozi wetu wa kitaifa kwa mfano falsafa ya R4 (Reconciliation - Maridhiano au upatanisho, Resilience - ustahimilivu, Reforms - mageuzi na Rebuilding - ujenzi mpya wa Taifa) iliyoasisiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu, yenye lengo la kuimarisha amani na mshikamano wa kitaifa.

Ndugu Wajumbe na wageni waalikwa,

Reconciliation yaani maridhiano ni muhimu sana kwani yanaleta uponyaji. Lakini lazima tujiulize, tunaponya nini na nani wanahusika katika huo uponyaji? Resilience – ustahimilivu hasa wakati wa matatizo mathalani tukio lililotokea Hanang, Manyara si tu wananchi wameonyesha ustahimilivu, bali makundi yote yalitoa msaada kwa waathirika na kuwasaidia wananchi wa eneo hilo. Hii ni alama ya upendo na ustahimilivu wakati wa matatizo. R ya tatu "Reforms" yaani mageuzi tunazungumzia kwenda kwenye mageuzi ya kweli katika nyanja zote. Tusikubali leo ikawa kama jana, na jana kama juzi, lazima kesho yetu ioneshe kwamba tulivuna kitu leo kilichotokana na tulichovuna jana. Kwenye R ya mwisho ya ujenzi

mpya wa taifa, hapa tumekumbushwa tunu zetu - utu, umoja, udugu, maelewano, ushirikiano, pamoja na amani.

Ndugu Wajumbe na wageni waalikwa,

Mwaka huu taifa linaingia katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na mwaka kesho kwenye Uchaguzi Mkuu, hivyo nitoe rai kwenu wana habari mjikite sana kutoa elimu ya mpiga kura kwa wananchi kwa lengo la kuwajengea uelewa wa sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza mchakato mzima wa uchaguzi pamoja na umuhimu wa kushiriki katika chaguzi. Ni matumaini yangu kuwa mtatumia maarifa mtakayoyapata katika mkutano huu kuwahamasisha wananchi kutumia haki yao ya kikatiba katika kujitokeza na kushiriki kuchagua viongozi wao.

Ndugu Wajumbe na wageni waalikwa,

Aidha, nitumie fursa hii kuwakumbusha kuwa pamoja na kwamba mitandao ya kijamii imefungua dirisha la mawasiliano hasa kwa vijana, baadhi ya maudhui katika mitandao hiyo hayana ukweli na mengine hayazingatii utu na heshima ya binadamu. Ni kwa muktadha huu ninawaomba mtambue kuwa nyinyi ni nguzo muhimu ya kuwapa Watanzania habari sahihi, hivyo tumieni mafunzo mliyoyapata kuongeza weledi na ubunifu katika kuhabarisha wananchi ili kuondoa uwezekano wa kuonea kwa taarifa za uongo na uzushi hasa katika ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia ambapo wananchi wengi wanaitumia mitandao ya kijamii kama njia mojawapo ya kupata habari.

Ndugu Wajumbe na wageni waalikwa,

Serikali inatambua mchango wa sekta ya habari ndio maana iliamua kila Wizara, Idara na Mashirika yake yawe na Maafisa Habari lengo kubwa likiwa ni kuhakikisha kwamba habari muhimu zinawafikia wananchi. Ni katika muktadha huu nawaomba mshirikiane na TBC na kuandaa vizpindi vyenye mavuto kwa wananchi na vinavyoelezea juhudi za Serikali za kuwafikishia wananchi huduma huko waliko. Aidha, ni matumaini yangu kuwa mkutano huu utawaandaa na kuwapa mbinu za kutayarisha maudhui kwa ajili ya vyombo na majukwaa mbalimbali ili kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu shughuli zinazofanywa na Serikali yao.

Ndugu Wajumbe na wageni waalikwa,

Rai yangu kwenu mtumie Mkutano huu ili vipindi mtakavyo viandaa na taarifa mtakazotoa kwa umma zilenge katika kujibu kero mbalimbali za Watanzania. Napenda tena kuwashukuru wadhamini kwa kuona umuhimu wa kudhamini mkutano huu. Niwashukuru washiriki kwa kuhudhuria kwa wingi, na mwishio kabisa niipongeze tena TBC kwa kuandaa na kuratibu mkutano huu,

Baada ya kusema hayo naomba nitamke kuwa mkutano wa 108 wa Watayarishaji wa Vipindi vya Elimu kwa Umma unaofanyika Jijini Mwanza, umefunguliwa rasmi.

!!!ASANTENI!!!